

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

TANGAZO LA ZABUNI

QUOTATION (NUKUU YA BEI) Na. LGA/018/2020/2021/NCS/17 MAOMBI YA KUPANGISHA ENEO LA KIOSKI CHA VINYWAJI NA SEHEMU YA NYAMA CHOMA DCC-PARK-DRIMP

Halmashauri ya Jiji inakaribisha maombi ya kupangisha Eneo la Kioski cha vinywaji na sehemu ya nyama choma katika eneo la DCC Park DRIMP. Mwombaji awe na uwezo wa kulipa fedha ya dhamana ya miezi mitatu ya malipo ya eneo la kupanga la kutolea huduma tajwa hapo juu.

Zabuni hii iko wazi kwa wazabuni wote wenye ujuzi wa kuendesha biashara ya vinjwaji na nyama choma. Kila mwombaji atatakiwa kufika katika eneo la DCC Park DRIMP lililopakana na soko la Mchikichini Ilala Boma kwa ajili ya kuona eneo husika kabla ya kuleta maombi. Zoezi la ukaguzi litafanywa kuanzia tarehe 05 mwezi wa Februari, 2021 saa 3:00 Asubuhi hadi saa 9:00 Alasiri.

Fomu ya maombi ya Zabuni iliyoandikwa kwa Lugha ya Kiswahili itapatikana Ofisi ya Menejimenti ya Manunuzi, iliyopo gorofa ya kwanza Jengo kuu kwenye makutano ya barabara ya Morogoro na Sokoine Drive Dar es Salaam. Fomu hiyo itauzwa kwa fedha za Kitanzania **20,000/=** (Shilingi Elfu Ishirini) ambayo haitarudishwa. Fomu hiyo itajazwa na mwombaji zabuni na kuweka kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na kutumbukizwa kwenye sanduku la Zabuni, lililopo kwenye Ofisi ya Menejimenti ya Manunuzi Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ikiwa imetaja Zabuni **LGA/018/2020/2021/NCS/17**, kwa anuani ifuatayo

Mkurugenzi Jiji,
Halmashauri ya Jiji,
S.L.P. 9084,
DAR ES SALAAM

Mwisho wa kuwasilisha Zabuni ni Jumatano tarehe 10 Februari, 2021 saa nane mchana na zabuni itafunguliwa siku hiyo hiyo na muda huo huo kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Jiji (Board Room). Wazabuni au wawakilishi wanakaribishwa kuhudhuria kikao cha ufunguzi.

Zabuni itakayochelewa muda wa ufunguzi haitasomwa wakati wa ufunguzi au itakayotumwa kwa njia ya mtandao haitakubalika.

**MKURUGENZI
HALMASHAURI YA JIJI**